# HALMASHAURI YA MJI WA BABATI.

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MENEJIMENTI KILICHOFANYIKA TAREHE 18.01.2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURIYA MJI WA BABATI.

**MAHUDHURIO**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. | Faustine | N. | Masunga | Kaimu Mkurugenzi wa Mji | M/Kiti |
| 2. | Bw | Mrisho | A. | Mlela | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi. | Katibu |
| 3. | Bw | Khamis | J. | Katimba | Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji. | Mjumbe |
| 4. | Bw | Mathias | M. | Mkumbo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 5. | Bw | Azael | A. | Mchomvu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano. | Mjumbe |
| 6. | Bi. | Amina | A. | Masood | Mkuu wa Idara ya M/Jamii. | Mjumbe |
| 7. | Bw | Emmanuel | J | Shimi | Mkuu wa Idara yas Fedha na Biashara. | Mjumbe |
| 8. | Bw. | Mohamed | K | Msalu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi. | Mjumbe. |
| 9. | Bi. | Pascalina | H. | Lowokelo | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari | Mjumbe |
| 10. | Bw | Osmund | J. | Komba | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Mjumbe |
| 11. | Bw | Daniel | A. | Luther | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | Mjumbe |
| 12. | Bw. | Simon | R. | Mumbee | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi. | Mjumbe |
| 13. | Dkt | Halima | H. | Mangiri | Mganga Mkuu wa Mji | Mjumbe |
| 14. | Bw. | Aretas | H. | Laurent | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu | Mjumbe |
| 15. | Bw. | Osward | F. | Macha | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi. | Mjumbe |
| 16. | Dkt | Fatuma | A. | Mkombozi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi. | Mjumbe |
| 17. | Bw | Frank | I. | Msuya | Katibu wa Kamati. | |



Scanned with CamScanner

18. Bi. Restituter A. Makuru Katibu wa Kamati.
19. Bw. Hassan A. Mangalili Katibu wa Kamati.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.116/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**
Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:00 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA. 117/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA**
Wajumbe walipokea na kuridhia agenda 15 zijadiliwe kwenye kikao.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.118/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 10.12.2021**
Kabla ya kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 10.12.2021 yalifanyika masahihisho yafuatayo:

**Ukusara namba 2 muhtasari BTC/TMT09.MUHT. NA.100/2021/2022**
Neno Agenda kumina tatu lisomeke; Agenda namba kumi na tatu.

Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliuthibitisha muhtasari kuwa sahihi.

Mwenyekiti na Katibu waliusaini muhtasari pamoja na masahihisho yake kuwa kumbukumbu sahihi ya ofisi.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.119/2021/2022: KUPITIA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI**
Taarifa ya mihtasari ya Kamati za kudumu za Halmashauri katika vikao vya robo ya kwanza 2021/2022 iliwasilishwa kwa Wajumbe kama ifuatavyo:

1. Kamati ya Fedha na Uongozi muhtasari wa tarehe 20.12.2021.
2. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira muhtasari wa tarehe 18.10.2021.
3. Kamati ya Huduma za Jamii muhtasari wa tarehe 22.10.2021
4. Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 18.10.2021
5. Muhtasari wa Baraza la Madiwani la tarehe 1-2/11/2021

Wajumbe walisoma taarifa za mihtasari na kufanyia marekebisho sehemu zilizokuwa na dosari. Menejimenti iliridhia taarifa ya mihtasari hiyo iwasilishwe kwenye kamati husika.



Scanned with CamScanner

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.120/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI DESEMBA 2021**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha kwa wajumbe taarifa ya Mapato na matumizi ya mwezi Desemba 2021. Alieleza kuwa, mwaka 2021/2022 Halmashauri imekadiria kukusanya Tshs.26,476,836,900:00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mapato halisi ya Halmashauri mwezi Desemba 2021 ni Tshs:1,846,249,067:53

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Mapato halisi katika vyanzo vya ndani mwezi Desemba 2021 ni Tshs: 132,884,458,.66
2. Mapato halisi ya Ruzuku ya Mishahara mwezi Desemba 2021 Tshs.1,309,225,300.00
3. Mapato halisi ya Ruzuku ya Matumizi mengineyo mwezi Desemba 2021 Tshs.77,858,539.65
4. Mapato halisi ya Ruzuku ya Elimu Msingi bila ada mwezi Desemba 2021 Tshs.19,691,217.41
5. Mapato halisi ya Ruzuku ya Elimu Sekondari bila ada mwezi Desemba 2021 Tshs: 42,624,049.00
6. Ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa mwezi Desemba 2021 Halmashauri imepokea Tshs: 161,992,395.88

**MATUMIZI**

Mwezi Desemba 2021 Halmashauri imetumia Tshs: 2,244,363,687:90 kwa mchanganuo ufuatao:-

a) Uendeshaji wa Halmashauri fedha za ndani Tshs.83,183,340:00

b) Fedha za vyanzo lindwa Tshs.121,664,323.98

c) Miradi ya Maendeleo fedha za ndani Tshs.50,888,435.00

d) Ruzuku ya Mishahara Tshs1,309,425,300.00

e) Mkopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu Tshs.35,000,000.00

f) Ruzuku ya Matumizi Mengineyo Tshs.89,595,240.00



Scanned with CamScanner

g) Elimu bila Ada Tshs.42,624,048.92

h) Matumizi ya fedha za miradi mbalimbali Tshs. 511,983,000.00

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuelekeza yafuatayo;

1. Ziendelee doria za usiku kukagua vitabu vya kusajili wageni kwa ajii ya kufichua udanganyifu.
2. Kila kosa litakalobainishwa liadhibiwe na kutekelezwa..
3. Tarehe 25.1.2022 Menejimenti ijulishwe kwenye kikao kazi hatua za utekelezaji wa adhabu kwa wadaiwa sugu wa nyumba za kulala wageni waliokaidi kulipa faini.
4. Taarifa ya mikakati ya kukusanya mapato ya vyanzo vya ndani vilivyolivyokusanywa chini ya 50% itakuwa ikijadiliwa kwa awamu katika vikao kazi.
5. Kamati ya wataalam ya mapato ianze kufanya vikao vyake kila juma

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.121/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI KUHUSU**

**01. MPANGO WA MANUNUZI WA HALMASHAURI ROBO YA PILI 2021/2022**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aliwasilisha taarifa kwa wajumbe.

Alitaja kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Dsemba 2021 kama ifuatavyo:

1. Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ilifanya vikao viwili vya kutekeleza kazi na majukumu yake.
2. Yamefanyika manunuzi mtambuka ya Idara na Vitengo vya Halmashauri yenye thamani ya Tshs.371,080,114:00

Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa.

**02. MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI 2021/2022**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa kwa wajumbe.

Mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Mji wa Babati ilikadiria kupata na kutumia Tshs,.9,805,828,762:00 kutekeleza bajeti ya maendeleo.



Scanned with CamScanner

Chanzo cha fedha hizo ni ruzuku kutoka serikali kuu na vyanzo vya ndani vya Halmashauri.

Hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea Tshs.3,111,371,375 kutoka katika vyanzo mbalimbali na zimetumika Tshs.2,344,837,649:00 sawa na 23% ya lengo la matumizi ya bajeti ya maendeleo Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuridhia kwa hatua zaidi kwenye kikao cha kamati ya Fedha na Uongozi.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.122/2021/2022:UBORESHAJI MIUNDOMBINU YA MASOKO YA MIFUGO**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi alifahamisha wajumbe kwamba, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji imepokea barua Kumb. Na.BC/165/334/01/P50 ya tarehe 20.8.2021 kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa ikirejea maelekezo ya Katibu Mkuu kwamba:-

1. Serikali inatekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo hai katika masoko ya mifugo.
2. Lengo ni kudhibiti mifugo katika mnada, kukagua afya za mifugo na kukusanya mapato ya Serikali kwa ufanisi.
3. Serikali imetoa fedha za kuboresha mazingira ya mnada wa Gendi Tshs.269,000,000/-
4. Kazi itatekelezwa kwa awamu mbili.

Wajumbe walipokea taarifa na kuelekeza:-

1. Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili afuatilie Hati miliki ya eneo la Mnada wa Gendi kukidhi matakwa ya mwongozo wa matumizi ya fedha zilizotolewa.
2. Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi aombwe kibali cha kupandisha hadhi mnada wa Gendi baada ya maboresho kukamilika.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.123/2021/2022: MRADI WA JENGO LA HUDUMA YA DHARURA (EMD) LA HOSPITALI YA MJI WA BABATI.**

Mganga Mkuu wa Mji alifahamisha wajumbe kwamba, Halmashauri ya Mji wa Babati imepokea Tshs.390,000,000:00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:-



Scanned with CamScanner

1. Ujenzi wa nyumba ya Mganga katika Kituo cha afya Mutuka Tshs.90,000,000
2. Ujenzi wa jengo la huduma za dharua (EMD) katika Hospitali ya Mji Tshs.300,000,000:00
3. Fedha hizo zimetolewa na mwongozo wa awali kwamba atumike mkandarasi kutekeleza miradi hiyo.
4. Tarehe 13.01.2022 Katibu Mkuu TAMISEMI alitoa mwongozo mwingine kubadili maelekezo ya awali kwamba miradi itekelezwe kwa kutumia 'Force Account'

Wajumbe walipokea taarifa na kuelekeza wataalam wa Force Account' kufanya maandalizi ya kutekeleza miradi hiyo.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.124/2021/2022: MAPENDEKEZO YA KUTOA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI**

Kaimu Mkuu wa Idara ya M/Jamii aliwasilisha taarifa kwa wajumbe. Alieleza kuwa, vikundi kumi (10) vya Wajasiriamali vimekidhi vigezo vya kupatiwa mikopo kati ya vikundi kumi na mbili (12) vilivyowasilisha maombi kwa Mkurugenzi wa Mji.

Kati ya vikundi hivyo kumi (10) vikundi viwili (02) ni vya Wanawake, vikundi saba (7 ) ni vijana na kimoja (01) ni cha watu wenye ulemavu.

Vikundi kumi vilivyokidhi vigezo kupitia mchujo wa wataalam wa Idara vimeomba mkopo wenye thamani ya Tshs.140,136,,000:00 kama ilivyo katika jedwali hapo chini.

| NA | JINA LA KIKUNDI | OMBI KIKUNDI | KAMATI YA MIKOPO | MENEJIMENTI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | RAFIKI NA MAENDELEO | 16,000,000 | 8,622,000 | 8,622,000 |
| 2 | THE BRIGHT | 6,000,000 | 6,000,000 | 6,000,000 |
| 3 | VIJANA UMOJA NI NGUVU | 24,980,000 | 24,990,000 | 24,990,000 |
| 4. | BARAKA SAWE | 11,035,000 | 5,000,000 | 5,000,000 |
| 5 | MIRAWA | 24,000,000 | 5,000,000 | 5,000,000 |



Scanned with CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | NYEGEZI | 24,960,000 | 24,990,000 | 24,990,000 |
| 7. | WANAKAKOI | 35,000,000 | 25,666,000 | 25,666,000 |
| 8. | AMKA | 12,480,000 | 22,480,000 | 22,480,000 |
| 9 | TANZANIGHT | 14,967,600 | 14,967,600 | 14,967,600 |
| 10 | BODABODA MAISAKA KATI | 12,480,000 | 12,480,000 | 12,480,000 |
| **JUMLA** | | **181,913,000** | **140,136,000** | **140,136,000** |

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuridhia mchakato wa maombi ya kutoa mkopo kwa hatua za maamuzi katika Kamati ya Fedha na Uongozi

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.125/2021/2022: TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI 2021/2022**

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa kwa wajumbe.

Alitaja changamoto katika ukaguzi uliotekelezwa katika robo ya pili 2021/2022 kama ifuatavyo:-

1. Wajumbe wa Kamati za 'Force Account' hawana sifa za kutekeleza majukumu ya kamati.
2. Wajumbe wa Kamati za 'Force Account' wameshindwa kufanya tathmini (Evaluation) kuwapata wazabuni wenye sifa.
3. Kuna ukiukwaji wa Sheria, Kanuni unaofanywa na Kamati za 'Force Account' jambo linalosababisha ucheleweshaji wa miradi, kufanya maamuzi bila vikao na hifadhi duni ya nyaraka za mradi mfano hai ni kata ya Maisaka hivyo kamati zivunjwe na kuundwa upya.
4. Zifuatiliwe na kurejeshwa kwenye jalada nyaraka za mradi wa ujenzi wa chumba cha darasa katika shule ya msingi Singu.
5. Miradi ya afya itakayotekelezwa izingatie mbinu na maelekezo yaliyofanikisha miradi ya UVUKO-19.

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili kama ifuatavyo:-

1. Dosari nyingi zinajitokeza kwa sababu ya tofauti kati ya Viongozi wa Jamii na wataalam. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ijulishwe jambo hili ili kuelekeza viongozi wa Jamii kupokea ushauri wa wataalam.



Scanned with CamScanner

2. Zifanyike jitihada za ziada kudhibiti mapaoromoko ya ardhi katika korongo mkabala na eneo la ujenzi wa Kituo cha afya Maisaka..
3. Menejimenti imeridhia ushauri wa Mkaguzi wa ndani wa kuvunja kamati zote za 'Force Account ' na kuziunda upya.
4. Menejimenti imeunda timu ya Wataalam ya kufuatilia kamati za 'Force Account', kuhakiki mapungufu na kuchukua hatua za kurekebisha makosa kwenye nyaraka. Wataalam: Mhandisi wa Mji, Mganga wa Mji, Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji - Kiongozi, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Mkuu wa Idara ya Elimu Elimu . Timu itaanza kazi kata ya Maisaka na tarehe 25.1.2022.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.126/2021/2022: MAPENDEKEZO YA MAPITIO YA BAJETI YA HALMASHAURI 2021/2022**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha kwa wajumbe ombi la kutumia Tshs.50,000,000:00 za miradi ya maendeleo katika bajeti ya mwaka 2022/2023 kwenye kutekeleza kazi zifuatazo:-

1. Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule shikizi ya Ayabadney Tshs.10,000,000:00
2. Kuezeka kituo cha Afya Nangara Tshs.5,000,000.00
3. Kujenga vyumba viwili vya madarasa katika shule mpya ya sekondari ya Maisaka Tshs.20,000,000:00
4. Kumalizia nyumba ya mwalimu shule ya Msingi Nakwa Tshs.15,000,000:00

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuridhia pendekezo hilo kwa hatua za maamuzi katika kikao cha kamati ya Fedha na Uongozi.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.127/2021/2022: PENDEKEZO LA KUHUISHA MPANGO WA MANUNUZI**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aliwasilisha kwa wajumbe ombi la kuhuisha Mpango wa manunuzi wa Halmashauri wa mwaka 2021/2022.

Mpango unahuishwa kutokana na fedha zilizoletwa nje ya bajeti ya mwaka 2021/2022 Tshs.1,520,000,000.00 zinazobadilisha Mpango wa manunuzi wa Halmashauri kutoka Tshs.9,332,294,037 kuwa Tshs.10,852,294,032



Scanned with CamScanner

Fedha zilizoletwa zimepangwa katika miradi ifuatayo:

i. Kujenga nyumba ya watumishi Kituo cha Afya Mutuka Tshs.90,000,000.00

ii. Ukamilishaji wa kituo cha afya Mutuka Tshs.300,000,000.00

iii. Ujenzi wa jengo la huduma za dharura Hospitali ya Mji Tshs.300,000,000.00

iv. Ujenzi vyumba vya madarasa UVIKO 19 Tshs.360,000,000.00

v. Ujenzi wa shule mpya ya sekondari Himiti Tshs.470,000,000.00

Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia ombi la kuhuisha Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri wa mwaka 2021/2022 kwa hatua zaidi za maamuzi katika kamati ya Fedha na Uongozi.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.128/2021/2022: MIRADI INAYOTEKELEZWA KATIKA UWANJA WA KWARAA**

**01. UENDELEZAJI WA UJENZI WA VIBANDA UWANJA WA KWARAA OKTOBA HADI DESEMBA 2021**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji alieleza, hadi tarehe 31.12.2021 wadau 143 walikuwa wamepatiwa maeneo ya ujenzi wa vibanda vya biashara.

Kazi ya ujenzi wa ukuta wa kutenganisha eneo la shule ya msingi Babati na Oysterbay upo katika hatua ya kukamilisha kazi.

Tarehe 04.11.2021 maeneo wazi yasiyoendelezwa yalitangazwa na wadau 10 wajilitokeza kupatiwa maeneo 10. Maeneo ambayo bado wazi yanaandaliwa utaratibu wa kujengewa ukuta na Halmashauri

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili kama ifuatavyo:-

1. Uandaliwe mpango kazi wa kukamilisha kazi katika Uwanja wa Kwaraa ili uwanja uanze kutumika.
2. Ikamilishwe kazi ya kukadiria gharama za ujenzi wa vibanda ili wadau waweze kusaini mkataba na kulipa ushuru.

**02. UJENZI WA VIBANDA JIRANI NA KIZIMBA CHA TAKA**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu alieleza wajumbe kwamba ujenzi wa vibanda vya biashara karibu na kizimba cha taka unaweza kusababisha madhara yafuatayo:



Scanned with CamScanner

1. Kuingilia miundombinu ya kizimba.
2. Wadau wa biashara kuvamiwa na mazingira yasiyosalama wadudu kutoka kwenye taka.
3. Harufu ya taka ni kero kwa wadau

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili kama ifuatavyo:

1. Ukuta unaojengwa kutenganisha eneo la shule na Uwanja wa Kwaraa uendelezwe kutenganisha eneo la kizimba na eneo la biashara.
2. Eneo la vibanda vitatu (3) kuelekea kwenye kizimba libaki wazi kulinda afya ya wadau jirani na kizimba.
3. Kikao kijacho Menejimenti ifahamishwe namna Halmashauri inavyonufaika na matumizi ya eneo jirani na Bar ya Kabila

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.129/2021/2022: TAARIFA ZA IDARA NA VITENGO**

Taarifa za utekelezaji wa Idara na Vitengo ziliawasilishwa kwa wajumbe na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

1. Uandaliwe utaratibu wa kuzipongeza shule za sekondari zilizofanya vizuri katika mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2021.
2. Menejimenti ilipitia taarifa za utekelezaji za Idara na Vitengo na kuridhia ziwasilishwe kwenye vikao vya kamati za kudumu za Halmashauri.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.130/2021/2022: TAARIFA YA MAFUNZO YA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO:**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi alifahamisha wajumbe kwamba tarehe 05/01/2022 yalifanyika mafunzo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara ambayo Mkurugenzi wa Mji, Mwenyekiti wa Halmashauri na Wataalam wa mifugo wa Halmashauri ya Mji walialikwa.

Lengo la mafunzo ni kuwezesha wataalam taratibu za kuhamasisha jamii kuhusu zoezi la kutambua, kufuatilia na kusajili mifugo kwa kutumia mfumo wa Kielekroniki.

Ni mpango wa Kitaifa wa kusajili mifugo na kuivalisha Hereni zenye namba za utambuzi zinazoingizwa katika mfumo wa Kielekroniki.



Scanned with CamScanner

Zipo fursa mbili za kutekeleza kazi hiyo;-

1. Halmashauri kutumia wataalam wake
2. Kutangaza zabuni na kumpata Mkandarasi

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kushauri mradi utekelezwe kwa kutumia Mkandarasi kwa sababu ya uhaba wa wataalam.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.131/2021/2022: MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa kwa wajumbe.

Alieleza Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Sigino imewasilisha ombi kwa Mkurugenzi la kubadili matumizi ya Tshs.10,000,000:00 zilizopangwa kujenga ofisi ya kata zielekezwe kwenye ujenzi wa bweni la pili la shule ya sekondari ya Sigino.

Ombi limetokana na kuwepo kwa miradi inayotekelezwa kwa wakati mmoja ambayo inachangiwa na jamii hivyo kusababisha mzigo mkubwa.

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuridhia ombi la badiliko la matumizi ya fedha Tshs10,000,000:00 kwa hatua ya maamuzi katika Kamati ya Fedha na Uongozi

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.132/2021/2022: HITAJI LA KUWEZESHWA NGAZI YA KATA**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa kwa wajumbe

Alieleza, ufanisi wa majukumu ya Halmashauri hususani yale yanayoanzia ngazi za jamii yanategemea wataalam wanaofanya kazi ngazi za msingi.

Ngazi ya kata inatakiwa kujengewa uwezo kubadili mfumo unaotumika kwa sasa wa mtaalam kutekeleza kazi zake mwenyewe katika eneo lake la kisekta. Mfumo huu unadhoofisha mafanikio na uwajibikaji wa haraka katika kutoa huduma na majibu tarajiwa. Yafanyike maboresho kwa kuunda timu ya wataalam (Menejimenti ya kata) itakayoongozwa na Mtendaji wa Kata ili kupanga na kutekeleza kazi zao kwa ushirikiano.



Scanned with CamScanner

Mahitaji muhimu:-

1. Ngazi ya Kata wawe wakipatiwa shajala
2. Vitendea kazi muhimu vya ofisi kama kompyuta na printa
3. Mafuta kwa ajili ya kuwezesha pikipiki au ufuatiliaji.
4. Motisha ili kuongeza bidii katika kazi
5. Mshauri wa karibu katika kutatua changamoto wanazokutana nazo.

Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia kuwa itengwe bajeti hata kama ni kidogo kwa hatua ya kuanza maboresho katika ngazi ya kata.

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.133/2021/2022: MPANGO WA SERIKALI WA KURASIMISHA MAKAZI**

Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili aliwasilisha taarifa kwa wajumbe.

Alieleza, Halmashauri ya Mji wa Babati ni miongoni mwa Halmashauri zitakazo patiwa fedha za kurasimisha makazi. Fedha zilizopangwa kutolewa na serikali katika Halmashauri ya Mji ni Tshs.250,000,000. Kiwango cha fedha hizo kinatarajiwa kuwezesha urasimishaji wa makazi 2500.

Muda wa utekelezaji ni miezi sita na kipaumbele kinapendekezwa kuwa Mtaa wa Sawe na Nangara Kati maeneo yaliyoiva kwa urasimishaji.

Wajumbe walipokea taarifa wakaijadili na kuelekeza, Idara ya Ardhi na maliasili iandae mpango kazi na kuainisha vipengele vifuatavyo:-

1. Gharama za upimaji, muda wa marejesho na namna mwanchi atakavyorejesha.
2. Mbinu za kusimamia mkataba endapo atatumika mkandarasi hadi kufanikisha kazi inayokusudiwa.
3. Endapo Halmashauri itapima yenyewe itanufaika na nini.
4. Faida itakayopatikana kwa kutumia vifaa vya upimaji vya Halmashauri katika mkataba na mkandarasi
5. Taarifa ya mpango kazi iwasilishwe kikao kazi cha tarehe 25.1.2022



Scanned with CamScanner

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.134/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwepo na Mengineyo

**BTC/TMT.12/MUHT.NA.135/2021/2022KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 11:30 Jioni kwa kuwashukuru wajumbe kwa ushiriki mazuri katika mjadala.

**UMETHIBITISHWA NA**

........................................
*Bw.M.A. Mlela*
**KATIBU**

........................................
*Bw. Faustine N. Masunga*
**MWENYEKITI**

10/2/2022
........................................
**TAREHE**



Scanned with CamScanner